


# FADev

TAASISI YA KUENDELEZA UCHIMBAJI MDOGO

## Malengo Yetu

- Sekta Rasmi na Halali Kisheria
- Sekta Adilifu na inayojali Mazingira
- Ushiriki wenye tija wa wanawake katika sekta ya uchimbaji mdogo
- Biashara Endelevu ndani na nje ya Sekta ya uchimbaji mdogo
- Mijadala Shirikishi na uimarishwaji wa Taasisi



## Historia Fupi

Taasisi ya kuendeleza Uchimbaji Mdogo (FADev) ni shirika lisilo la kiserikali lililosajiliwa chini ya Sheria ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ya mwaka 2002, katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania yenye namba ya usajili 00NGO / R / 0251.

Kuanzishwa kwa FADev kulitokana na utafiti na pia mijadala mbali mbali ya kitaifa ambayo ilithibitisha kuwepo uhitaji wa kuwa na taasisi ambayo itashughulikia masuala ya uchimbaji mdogo wa madini nchini.

Ripoti za utafiti na ripoti ya mijadala mbalimbali iliyofanyika kwa kuongozwa na Taasisi ya Kimataifa ya Mazingira na Maendeleo (IIED) kwa kushirikiana na Hakimadini (shirika lisilo na kiserikali Tanzania) zinapatikana kwenye tovuti yetu. Unaweza kupakua ripoti hizi kupitia www.fadev.or.tz.

**Dira Yetu**

Kuhakikisha kwamba shughuli za sekta ya uchimbaji mdogo wa madini nchini Tanzania ni adilifu, shirikishi na endelevu.

**Dhima Yetu**

Kukuza uchimbaji mdogo wa madini unaowajibika na endelevu, ikiwa ni pamoja na kuongeza stadi za maisha miongoni mwa wachimbaji wadogo wa madini.

## Programu Zetu

Shughuli za Taasisi ya kuendeleza uchimbaji mdogo zinaongozwa na nguzo tano za suluhisho zilizotambuliwa kwenye mijadala kama ifuatavyo:



### 1. Kuboresha shughuli za kisheria na Mifumo ya Kurasimisha Sekta ya Uchimbaji Mdogo wa Madini

Kurasimisha na kuhalalisha sekta ya uchimbaji mdogo wa madini kunahitaji marekebisho ya sera zilizopo na mifumo ya kisheria, kuongeza ushiriki wa wadau na kupanua uelewa kupitia mifumo ya kisasa ya mawasiliano na uhamasishaji. Katika kufanikisha hili, FADev inahakikisha inakuwepo mifumo inayolenga kutenga ardhi iliyopimwa kwa ajili ya shughuli za uchimbaji mdogo wa madini, taarifa muhimu za kijiolojia, huduma za ugani na motisha kwa shughuli za uchimbaji mdogo ulio rasmi na halali.

FADev inafanya kazi na wadau mbali mbali ili kupata sera ya ardhi iliyo rafiki na njia rahisi ya upatikanaji wa leseni za uchimbaji mdogo wa madini. Kama kianzio, mchakato huu unahakikisha kwamba kuna ufafanuzi wa maneno yanayotumika kuelezea tasnia hii na hali tofauti ya viwango anuwai vya utendaji, haswa: uchimbaji mdogo wa madini, na uchimbaji wa madini kwa kiwango cha kati.

### 2. Kukuza Uchimbaji Mdogo unaojali mazingira na jamii

Marekebisho yenye lengo la kuboresha utendaji wa sekta ya uchimbaji mdogo ili uwe wenye tija na unaotunza mazingira yanapaswa kuhamasishwa ili kukuza dhana ya uchumi endelevu na usioharibu au kuchafua mazingira. Mara nyingi, hatua zinazochukuliwa kuhakikisha uchimbaji mdogo wa madini unawajibika zinalenga zaidi 'kukomesha' athari kwa mazingira na jamii zinazosababishwa na uchimbaji mdogo. Mbinu hizi bado hazijaleta matokeo yaliyolengwa. Mara nyingi, shughuli za uchimbaji mdogo wa madini zinatokana na hali duni kiuchumi ya wananchi wanaoishi kwenye maeneo yenye madini. Hali hii imesababisha sekta hii kutozalisha kulingana na matarajio ya wachimbaji. Hata hivyo, endapo sekta hii ya uchimbaji mdogo wa madini itasimamiwa ipasavyo, shughuli za uchimbaji mdogo zitaweza kuongoza katika kukuza uchumi na maendeleo ya jamii katika maeneo husika.



FADev imeanzisha programu mahususi kabisa ili kuangazia masuala yanayohusu Mazingira, Afya na Usalama. Programu hii inajumuisha shughuli nyingi, ikiwemo kuhamasisha shughuli za uchimbaji mdogo wa madini unaozingatia misingi ya kulinda afya za wachimbaji, usalama na pia kuzingatia kanuni za kutunza mazingira.

### 3. Kukuza Ushiriki wa Wanawake katika Sekta ya Uchimbaji Mdogo wa Madini

Mchakato wa maboresho ya sera zinazolenga kuwajengea uwezo kiuchumi wanawake katika sekta ya uchimbaji mdogo unapaswa kuzingatia mbinu suluhishi zinazogusa masuala ya kijamii, kisheria, kiuchumi, kiufundi, kitaaluma na kisiasa. Mbinu hizi hazipaswi kushughulikia tu changamoto mbalimbali zinazowakabili wanawake, bali zinapaswa kutambua michango ya wanawake walio kwenye sekta ya uchimbaji mdogo na kuwajengea uwezo zaidi. Kwa kufanya hivyo, mchango wa mwanawake utakuwa mkubwa na wenye umuhimu katika kukuza uchumi, kupanua wigo wa biashara, kushiriki vilivyo kwenye ngazi ya kufanya maamuzi yenye tija, na kufanya shughuli hizi kwa ufanisi.

Katika utendaji wake, FADev inafanya kazi ya kubaini na kutoa mapendekezo jinsi ya kutatua changamoto za kijinsia katika sera na kanuni za madini ili ziweze kutambua na kuainisha haki na sehemu ya mwanamke ndani ya tasnia ya uchimbaji mdogo wa madini.

### 4. Kuunga mkono ukuaji wa maendeleo na mazingira endelevu ya biashara ndani na nje ya shughuli za uchimbaji mdogo wa madini

Kwa kuzingatia uwezo mdogo wa kuendesha shughuli za uchimbaji mdogo kibiashara wa waendeshaji wa shughuli za uchimbaji mdogo wa madini kuzifanya shughuli hizi kiujasiriamali zaidi, FADev inaelekeza msaada wake kwenye maeneo kama upatikanaji wa huduma ya fedha, upatikanaji wa masoko, kukuza ujuzi wa kiufundi na teknolojia miongoni mwa wachimbaji wadogo wa madini na kutoa elimu



juu ya ustadi wa biashara na uongozi. Hivi ni vipengele muhimu katika kutambua thamani ya uchumi wa sekta hiyo. Jambo lingine la kutilia mkazo ni umuhimu wa kuwa na mpango wa biashara wa muda mrefu, ili kuwaandaa wachimbaji kuchangamkia fursa za kupanua wigo wa biashara endelevu katika maeneo mengine mbali na uchimbaji wa madini.

FADev inafanya kazi na wachimbaji wadogo wanaomiliki maeneo kihalali wenye leseni (PMLs) ili kuanzisha na kuenendeleza migodi ya mifano kama njia mojawapo ya kuhakikisha shughuli za uchimbaji mdogo ni endelevu na zinafanyika kwa njia salama kwa kuzingatia utunzaji wa mazingira. Migodi ya Mfano ni hatua muhimu ya kuonyesha mfano mzuri wa kuendesha shughuli za uchimbaji mdogo kibiashara zinazowajibika na endelevu.

### 5. Kukuza Majadiliano na Uwezeshaji wa Taasisi

Kufuatia majadiliano ya kitaifa yaliyowajumuisha wadau muhimu wa sekta ya uchimbaji mdogo nchini Tanzania, na uwezeshaji wadau katika ngazi ya chini na kitaifa, tunaamini kwamba ukuzaji wa majadiliano kati ya wadau inabaki kuwa kielelezo cha kipekee kwa FADev. Taasisi ya Kuendeleza Uchimbaji Mdogo itaendelea na mikakati ya kuwapatia mafunzo wadau mbalimbali, kubadilishana maarifa/uzoefu na kudumisha ushirikiano ili kufanikisha dira yetu ya kuwa na sekta ya uchimbaji mdogo wa madini nchini Tanzania ambayo ni adilifu shirikishi na endelevu.

FADev inajenga jukwaa la majadiliano linalotumia teknolojia ya kisasa kuhakikisha wadau mbalimbali wa uchimbaji mdogo wa madini walio ndani na nje ya Tanzania wanajadiliana na kubadilishana mawazo kuhusu uendelezaji wa uchimbaji mdogo. Jukwaa hili litatumika kama kitovu cha kupata taarifa mbalimbali za uchimbaji mdogo wa madini.

## Maadili yetu

- Uadilifu
- Uwajibikaji
- Usawa
- Ushirikishwaji
- Kushirikishana maarifa


**Mawasiliano**

FADev, Kitalu Namba 53
Barabara ya Chole, Msasani Peninsula
S. L. P 75419, Dar es Salaam – TANZANIA.
Ofisi: +255 747 474 291
Barua Pepe: info@fadev.or.tz
Tovuti: www.fadev.or.tz

fadevtz
FADevTz
Foundation for ASM Development